# KAULI YA WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA KUHUSIANA NA KUIBUKA KWA MAGONJWA YA MAZAO MBALIMBALI NA HASA UGONJWA MPYA WA MAHINDI NCHINI UJULIKANAO KWA JINA LA "MAIZE LETHAL NECROSIS DISEASE"

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge Na. 49 (1) - (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2003, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa kauli ya Serikali kuhusiana na kuibuka kwa magonjwa ya mazao mbalimbali na hasa ugonjwa mpya wa mahindi nchini unaojulikana kwa jina la **" Maize Lethal Necrosis Disease"**

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa nchi yetu imekumbwa na ugonjwa mpya unaoathiri mahindi. Ugonjwa huu unajulikana kama **" Maize Lethal Necrosis Disease"** (MLND). Ugonjwa huu ulionekana nchini Kenya mnamo mwezi Septemba, 2011 katika jimbo la Bomet lililopo katika bonde la Ufa. Baada ya taarifa hiyo Wizara ilianza kuchukua tahadhari na kuufuatilia kwa karibu.

Mwezi Agosti, 2012, watafiti wa mahindi wakiwa kwenye shughuli za kawaida za tathmini ya utafiti kwenye mashamba ya wakulima, walibaini mahindi yenye dalili za ugonjwa huu katika maeneo ya Mlangariri katika wilaya ya Arusha na Mbulumbulu Wilayani Karatu. Baada ya hapo kikundi kazi kiliundwa ili kufanya tathmini (survey) kwenye maeneo ya wilaya za mikoa ya Kanda ya Kaskazini

inayopakana na nchi ya Kenya. Katika tathmini hiyo, sampuli za mahindi yenye dalili za ugonjwa huo zilikusanywa na kupelekwa katika maabara. Matokeo ya uchunguzi huo yalionyesha kuwepo kwa ugonjwa huo na tayari umethibitishwa kuwepo katika mikoa ya Manyara, Simiyu, Mara, Arusha na Kilimanjaro.

Ugonjwa huu husababishwa na uwepo wa virusi vya aina mbili kwa pamoja ndani ya mmea wa mhindi. Muungano wa Virusi hivi ndani ya mhindi unahusisha virusi vijulikanavyo kwa jina la kitaalamu **“Maize Chlorotic Mottle Virus” (MCMV)** vikiwa kwa pamoja na **“Sugarcane Mosaic Virus” (SCMV)**. Hii inamaanisha kwamba, uwepo wa aina moja peke yake baina ya virusi hivi ndani ya mhindi hakusababishi kutokea kwa ugonjwa huu.

**Mheshimiwa Spika,** Tafiti zimebainisha kwamba ugonjwa huu husambaa kwa haraka kwa kuwa virusi vinavyosababisha ugonjwa huu vinaenezwa na wadudu wasambazaji **(vectors)** kama vile vidukari (aphids), dudugamba (beetles) na vithiripi (thrips). Wadudu hawa wanapeperushwa kirahisi na upepo kwa umbali mrefu na hivyo hatari ya ugonjwa huu kuenea katika maeneo mengi nchini ni kubwa.

## DALILI NA ATHARI ZA UGONJWA HUU

**Mheshimiwa Spika**, Ugonjwa huu huathiri mahindi katika hatua zote za ukuaji na dalili zinaanza wakati yanapofika urefu wa sentimeta 60. Dalili hizo ni pamoja na zifuatazo :-

1. Mmea mchanga unaposhambuliwa, majani yaliyoko katika ncha ya mmea maarufu kama moyo wa mahindi hufa (dead heart), na hivyo kusababisha mmea mzima kufa.

2. Majani ya juu kugeuka manjano na hatimaye hukauka kuanzia sehemu ya kati kuelekea pembezoni na kisha kugeuka rangi ya kahawia.

3. majani huendelea kukauka kuelekea kwenye shina.

4. ugonjwa huu ukiendelea sana shina na vifundo hukauka na kuwa rangi ya kahawia.

5. mahindi yaliyoshambuliwa huzaa machipukizi.

6. mbelewele hukosa chamvuo hivyo mmea kutozaa.

7. baada ya kuathirika kwa kiasi kikubwa na ugonjwa huu, mahindi hushambuliwa na ugojwa wa ukungu.

8. mahindi yaliyoshambuliwa huwa na magunzi madogo yenye mbegu chache au hayaweki mbegu kabisa.

Kasi ya mashambulizi ya ugonjwa huu na uharibifu unaweza kuwa mkubwa kiasi cha kufikia hadi hasara ya asilimia mia (100%).

## HATUA ZINAZOCHUKULIWA NA SERIKALI KUKABILIANA NA UGONJWA HUU

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupata taarifa ya kuwepo kwa ugonjwa huu katika nchi jirani ya Jamhuri ya Kenya, na maeneo ya kaskazini mwa Tanzania yanayopakana na Kenya, hatua zifuatazo zimechukuliwa na zinaendelea kuchukuliwa na Wizara:

a) Kuelimisha umma namna ya kutambua na kuudhibiti ugonjwa. Hatua za awali zilizochukuliwa ni pamoja na kufanya mikutano ya hadhara na wadau mbalimbali, kusambaza vipeperushi na mabango na kutoa taarifa magazetini. Aidha, wananchi wataendelea kuelimishwa kupitia vipindi vya Radio, Luninga na, kutoa mafunzo maalum kwa maafisa ugani vijijini.

b) Wizara kwa kusirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekamilisha Kanuni za kuzuia na kudhibiti ugonjwa huu **(*Prevention and Control Rules for Maize Lethal Necrosis Disease)*.** Kanuni hizi zinaelekeza kutosafirisha mahindi kutoka maeneo yaliyoathirika kwenda maeneo ambayo hayakuathirika yakiwa katika hali ya punje bali yakiwa yamesagwa na kusafirishwa yakiwa katika hali ya unga. Aidha, mtu yeyote atakayekiuka utekelezaji wa Kanuni hizi atachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria ya Hifadhi ya Mimea ya mwaka 1997, ikiwa ni pamoja na kuteketezwa kwa mahindi yatakayokamatwa kwa gharama za muhusika.

c) Kuendelea kufanya uchunguzi (survey) wa kitaifa ili kufahamu kiwango na maeneo yaliyoathirika na athari kwenye aina za mahindi yanayolimwa.

*d)* Kutafiti ili kugundua aina za mbegu za mahindi zenye ukinzani, na kupendekeza Udhibiti Husishi wa ugonjwa huu ***(Integrated Pest Management)****.*

e) Wizara kupitia Kituo cha Utafiti Mikocheni imewaongezea watafiti uwezo wa kufanya uchunguzi na utambuzi wa haraka kwa kununua VIFAA VYA UTAMBUZI (*Identification kit*).

**MBINU ZA KUKABILIANA NA UGONJWA HUU**

**Mheshimiwa Spika,** kuna mbinu zinazoweza kutumika kama tahadhari katika kukabiliana na ugonjwa huu ingawa hazitamaliza tatizo hili kabisa nazo ni kama zifuatazo :

i. Kupanda mbegu safi zilizothibitishwa ubora wake na Taasisi ya udhibiti wa ubora wa mbegu.
ii. Kudhibiti wadudu wanaosambaza ugonjwa huu kwa kupiga viuatilifu mahindi yanapokuwa shambani wakati yamefikia sentimita 60.
iii. Kung`oa mmea wowote unaoonyesha dalili za ugonjwa huu na kuuteketeza.
iv. Kufanya kilimo cha mzunguko kwa kubadilisha mazao ili kuvunja uzazi mzunguko wa virusi.
v. Kupanda mahindi mapema mwanzoni mwa msimu wa mahindi na kuhuisha mbinu za usafi wa shamba kwa kuondoa magugu yote shambani na kuongeza uhimili wa mmea dhidi ya ugonjwa kwa kutumia mbolea kwa vipimo sahihi na kwa wakati.

vi. Kutekeleza Sheria ya Hifadhi ya Mimea ya mwaka 1997 na kanuni zake za mwaka 1998

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua zilizokwishachukuliwa na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, unashauriwa kwamba suala la kutekeleza mbinu za kukabiliana na ugonjwa huu lichukuliwe kwa umuhimu unaostahili na wadau wote ili ugonjwa huu usisababishe janga la kitaifa. Aidha ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu imetayarisha vipeperushi vinavyoelezea ugonjwa huu ambavyo vimegawanywa kwa kila Mheshimiwa Mbunge.

**Mheshimiwa Spika,** Nakubaliana na Mheshimiwa Athumani Rashid Mfutakamba (MB) kwamba ni kweli nchi yetu imekumbwa na kasi kubwa ya milipuko ya magonjwa ya mazao mbalimbali yakiwemo muhogo, migomba, na mahindi. Magonjwa mbali mbali ya mazao yanasababishwa aidha na bakteria, virusi au ukungu. Magonjwa hayo ni pamoja na Unyanjano wa migomba (batobato kali ya muhogo michirizi kahawia ya muhogo na Maize Lethal Necrosis Disease" (MLND )

**Mheshimiwa Spika**, Virusi na bacteria husambazwa na wadudu mbalimbali kwa mfano dudugamba (Beetles), Aphids, Thrips nk. Wadudu hawa wanaruka na wanaotambaa na hupeperushwa na upepo umbali mrefu. Hata hivyo, magonjwa haya yameingia nchini katika vipindi tofauti. Serikali inaendelea kuchukua hatua za muda mfupi na mrefu ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa hayo ya mimea.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kutoa maelezo mafupii kuhusu wadudu aina ya vidukari (aphids), (beetles) na vithiripi (thrips). Wa**dudu hawa hawasababishi** sumu kuvu (aflatoxin) katika mazao, ila sumu Kuvu inasababishwa na vimelea vya ukungu vinavyojulikana kwa jina la kitaalamu kama *Aspergillus flavus*. Vimelea hivi vipo ardhini na mbegu zake (spores) zipo hewani. Mmea unapoathiriwa na virusi vinavyoenezwa na vidukari na vithiripi na kudhoofika ni rahisi vimelea vya ukungu kuingia na kuathiri mimea.

**Mheshimiwa Spika,** Tatizo la aflatoxin siyo geni hapa nchini hususan kwenye mazao ya karanga na mahindi, hii inatokana na hali ya kuhifadhiwa katika hali isiyo bora. Katika kulishughulikia suala hili **Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika,** inashirikiana na wadau wa ndani na wa Kimataifa ikiwemo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Viwanda na Biashara Wizara ya mifugo na maendeleo ya Uvuvi, TAMISEMI na Shirika la viwango la Taifa (TBS) katika kuweka mkakati wa kupunguza sumu kuvu katika vyakula. Kazi kubwa inayofanyika ni kuhamasisha wananchi walijue tatizo la sumu kuvu na jinsi watakavyodhibiti. Uhamasishaji unafanywa kwa kutoa vipindi kupitia luninga na radio , vipeperushi ili kueleza athari za sumu kuvu na jinsi ya kudhibiti vimelea hivi kuanzia shambani, hadi kwa mlaji.

**Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza awali, njia za kudhibiti ni pamoja na kufuata kanuni bora za kilimo na kukausha mazao vizuri kabla ya kuyahifadhi. Kwa kuwa tatizo hili linaweza kuondolewa kwa kufuata kanuni bora za kilimo na kuhifadhi, tunaamini kwamba mkakati huu wa

kuongeza uelewa utasaidia sana kupunguza tatizo hili kama tunavyofanya kwa ugonjwa wa UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika**, kuendelea kuibuka kwa magonjwa ya mazao mbali mbali ya chakula na biashara, husababishwa na mambo yafuatayo;-

a) Mabadiliko ya tabia nchi ambayo husababisha kubadilika kwa tabia za visumbufu na hivyo kusababisha kuenea kwa visumbufu hivyo pamoja na ugumu katika kuyadhibiti,
b) Kuongezeka kwa biashara za mazao / mimea kati ya nchi na nchi, ambapo mazao hayo huweza kuambatana na visumbufu visivyoonekana kwa macho na hivyo kuwa rahisi kwa ugonjwa kuweza kuingia nchini.
c) Wasafiri kutozingatia sheria za uingizaji wa mimea na mazao na hivyo kubeba vitu hivyo kwa kificho.

**Mheshimiwa Spika**, Hapo awali nimeeleza hatua zinazochukuliwa na Serikali kudhibiti ugonjwa mpya wa "Maize Lethal Necrosis“. Sasa naomba nieleze hatua zinazochukuliwa kudhibiti magonjwa mengine ambayo yamekuwepo hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ilipata taarifa ya kuwepo ugonjwa wa mnyanjano wa migomba katika nchi jirani ya Uganda, na kuanza kuchukua hatua za kudhibiti ugonjwa huu mara moja. Njia hizo ni kama ifuatavyo;-

a) Quarantine ya kuzuia migomba kuingia kutoka Uganda iliwekwa,

b) Elimu ilitolewa kwa maafisa mpakani pamoja na halmashauri juu ya ugonjwa huu.
c) Wilaya ambazo ziko mpakani na nchi ya Uganda (Wilaya za Karagwe, Misenyi na Bukoba Vijijini) ziliunda kamati za kudhibiti ugonjwa huu katika Vijiji vilivyoko mipakani.
d) Vipeperushi vinavyoelimisha namna ya kutambua, kujikinga na kudhibiti ugonjwa huu na sheria ya karantini viligawiwa katika ngazi ya Mkoa na Wilaya za Bukoba Vijijini na Karagwe.
e) Wataalam waliendelea kutembelea Wilaya za Bukoba Vijijini na Karagwe kuchunguza kama ugonjwa huu umeingia na kuwaelimisha wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya ugonjwa huo kuingia nchini, wataalamu wa Wizara pamoja na wale waliopo katika kituo cha Utafiti Maruku- Bukoba, walichukua hatua madhubuti juu ya kuwasaidia wananchi wa Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Geita na Kigoma kuweza kukabiliana ugonjwa huu kama ifuatavyo:

i. Kutoa elimu juu ya kudhibiti ugonjwa wa unyanjano wa migomba. Elimu hiyo ilitolewa kwa wataalamu (Wagani) wote mkoani Kagera.

   Vile vile elimu ilitolewa kupitia mikutano ya vijiji, radio, Televisheni, magazeti na video kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera.

ii. Machapisho ya vitini, majarida na vipeperushi vyenye ujumbe wa jinsi ugonjwa unavyoenea na namna ya kudhibiti magonjwa husika vimetengenezwa na

kusambazwa kwa wananchi mkoani kupitia maonyesho au sherehe za Nanenane, siku za wakulima (Farmer Field Days), Mashamba Darasa (Farmer Field Schools) na mikutano ya hadhara. .

iii. Kamati za kuhamasisha na kusimamia udhibiti wa ugonjwa wa unyanjano wa migomba (Mnyauko Bacteria-BXW) ziliundwa katika Wilaya za Muleba (Kata ya Ijumbi) na Bukoba (Kata ya Ruhunga) kama mfano wa namna jamii inavyoweza kupambana na ugonjwa huu. Katika Wilaya ya Muleba, kijiji cha Kabale ambako ugonjwa huu ulianzia walifanikiwa kudhibiti ugonjwa huu mwanzoni na sababu zilizopelekea mafanikio ni ushirikiano thabiti wa wahusika wote.

iv. Tangu mwaka wa 2009, Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Maruku kilianzisha shamba la mbegu mama la migomba Mbegu hizi husambazwa kwenye hatua ya pili ya uzalishaji wa mbegu (secondary nurseries katika Wilaya zote za Mkoa wa Kagera na Kibondo Mkoani Kigoma. Pia kituo kimefundisha wakulima njia ya haraka, rahisi na nyepesi ya kuanzisha kitalu cha mgomba katika Wilaya za Missenyi, Muleba, Ngara na Bukoba. Pia katika Wilaya hizi, Mashamba ya Mfano (banana demostrations) yamepandwa katika vijiji 15 chini ya usimamizi wa watafiti wa zao hili.

Pamoja na juhudi zinazofanywa na Wizara ya Kilimo na Taasisi zake, Wilaya ambako ndiko Waheshimiwa Wabunge mliko, zina jukumu kubwa kuhakikisha kuwa zinasimamia mapendekezo ya kitaalamu yaliyotolewa kama

nilivyoainisha hapo juu. Tuna ushahidi unaonyesha kwamba pale ambapo usimamizi umefanywa vizuri, ugonjwa huu ulipungua kwa kiwango kikubwa sana.

**Mheshimiwa Spika**, Ugonjwa wa bato bato kali katika zao la muhogo, ulitokea nchi ya jirani. Juhudi kubwa ilifanywa na inaendelea kufanywa na Wizara katika kupata suluhisho la ugonjwa huu. Wizara kupitia vituo vyake vya utafiti inaendelea kufanya utafiti wa mbegu kinzani dhidi ya ugonjwa wa batobato kali ya muhogo na tumefanikiwa kutoa mbegu bora nane (8) kwa ajili ya Kanda ya ziwa ambazo ni kinzani dhidi ugonjwa huu. Aina ya mbegu hizi ni Mkombozi, Meremeta, Kyaka, Isanzu, Rangimbili, Nyakafuro, Belinde na Suma. Pia uzalishaji wa mbegu kinzani dhidi ya ugonjwa huu unaendelea katika vituo vya utafiti vya Maruku na Ukiriguru. Pia mwaka jana mbegu nyingine 2 zinazovumilia ugonjwa huu zilitolewa kwa ajili ya Kanda ya Kati ambazo ni **Dodoma** na **Makutopora.** Mbegu hizi zinazalishwa katika kituo cha utafiti Homboro na Jitihada za kuzisambaza zinaendelea

**Mheshimiwa Spika**, Zao la muhogo limekuwa likikabiliwa pia na ugonjwa wa michirizi ya kikahawia (yaani - Cassava Brown Streak Disease). Ugonjwa huu unaathiri zao la muhogo katika ukanda wa Pwani hususani katika mikoa ya Tanga, Pwani, Dar-Es-Salaam, Lindi na Mtwara na umekuwa ukienea katika maeneo mbalimbali yanayolimwa muhogo kama kanda ya ziwa na nyanda za juu kusini. Wizara kupitia vituo vyake vya utafiti pamoja na mashirika ya kimataifa ya utafiti kama IITA inaendelea kufanya utafiti wa kugundua mbegu kinzani dhidi ya ugonjwa huu. Kwa mfano, mwaka jana, Wizara ilifanikiwa aina mbili za mbegu

ambazo ni **Pwani** na **Mkumba** zinazostahimili ugonjwa huu. Mbegu hizi kwa sasa zinazalishwa katika kituo cha utafiti cha Naliendele ili zisambazwe kwa wakulima.

**Mheshimiwa Spika,**Katika zao la kahawa, kumekuwa na magonjwa ya chulebuni (CBD), na kutu ya majani katika kahawa aina ya Arabika. Vile vile kumekuwa na tatizo la mnyauko fuzari katika kahawa aina ya robusta. Wizara kwa kushirikiana na wadau wa zao la kahawa, kupitia Taasisi ya utafiti wa kahawa (TaCRI) ilifanya utafiti na kugundua aina 15 za kahawa ya arabika zenye ukinzani na chulebuni na kutu ya majani, na aina 4 za kahawa ya robusta zenye ukinzani dhidi ya mnyauko fuzari wa kahawa. Kwa sasa Taasisi ya utafiti wa kahawa (TaCRI) kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya inaendelea kuzalisha miche bora ya aina hizo na kuisambaza kwa wakulima.

**Mheshimiwa Spika**, Hatua za kati na muda mrefu zinazochukuliwa na wizara ni pamoja na utafiti wa mbegu kinzani zinazoweza kuhimili magonjwa ikiwemo kutumia njia za bioteknologia.

Jukumu la kutumia mbinu zinazoshauriwa na wataalam katika kudhibiti magonjwa haya si la Serikali tu, bali ni la wadau wote mkiwemo Waheshimiwa Wabunge, Halmashauri za Wilaya na wakulima kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba magonjwa ya mimea niliyotaja yapo na kwamba Serikali inaendelea kuchukua hatua za kutokomeza magonjwa hayo ili kupunguza athari kwenye mazao yetu. Aidha nasisitiza kwamba hatua nyingine zinazochukuliwa ni

za Utafiti wa Kisayansi na mara nyingine zinachukua muda mrefu kuliko matarajio ya watu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kuwa watulivu na kufuata maelekezo wanayopewa na Wataalamu wa Kilimo na Wizara yangu itakuwa inatoa taarifa ya maendeleo ya utafiti wa njia za kutokomeza magonjwa ya mimea.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

Eng. Christopher Kajoro Chiza (MB)
**WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA**
25 JUNI 2013